## Maswali

1. Mfalme Dario alifanya nani kuwa mkuu wa wasimamizi kwa Ufalme wake?
2. Nani alionea Danieli wivu?
3. Wakuu wake walipata Danieli na makosa yoyote?
4. Danieli alifanya nini mara tatu kwa siku?
5. Wakuu wake walitaka Mfalme Dario afanye sheria gani mpya?
6. Danieli alifanya nini baada ya kusikia hiyo sheria mpya?
7. Mbona Mfalme Dario hakuweza kumwokoa Danieli kutoka kwa tundu la simba?
8. Nini ilifanyika kwa Danieli usiku huo?
9. Mfalme Dario alifanya nini kwa wakuu wake waovu?
10. Mfalme Dario alifanya sheria gani mpya?

## Majibu

1. Danieli alifanywa msimamizi mkuu.
2. Wakuu wa mfalme walionea Danieli wivu.
3. La. Wakuu wake hawakupata Danieli na makosa yoyote.
4. Danieli aliomba Mungu mara 3 kila siku. Alipiga magoti kwa dirisha.
5. Watu wowote wakiomba mungu kando na Mfalme kwa siku 30, watatubwa kwa tundu la simba.
6. Danieli alienda kwa dirisha lake na kuomba Mungu.
7. Sheria ya Wamedi na Waajemi haingeweza kubadilishwa.
8. Mungu alituma malaika wake. Malaika alifunga midomo ya simba na hawakumdhuru Danieli.
9. Mfalme Dario alitupa wakuu wake waovu ndani ya tundu la simba.
10. Kila mtu lazima aheshimu na kuogopa Mungu wa kweli mwenye aliokoa Danieli kutoka kwa simba.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 2 Mwaka wa 2**

# 84 Danieli katika tundu la simba

### Kwa Biblia

Danieli mlango wa 6

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu huponya wale wanaomwamini. Tusiwe na wivu

### Somo

Dario alikuwa Mfalme mpya. Mfalme Dario alichagua wakuu wake 120. Wakuu wake 120 walitawala sehemu mbali mbali katika Ufalme wa Wamedi na Waajemi. Mfalme Dario alichagua watu 3 kuwa juu ya wakuu wake 120. Danieli alikuwa mmoja wa wasimamizi watatu.

Danieli alikuwa mzee sana. Alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 80. Danieli alikuwa na ujusi mwingi. Alikuwa na hekima sana. Kawaida Danieli alikuwa akifanya mazuri. Alikuwa mwaminifu na wa kweli. Alikuwa msimamizi wa hekima. Mfalme Dario alifanya Danieli mkuu wa wasimamizi wa ufalme wake.

Wakuu wake walifanyia Danieli wivu. Hawakutaka awe mkuu wa wasimamizi. Wakuu wake walikaa wakimchunguza Danieli kila siku. Walijaribu kutafuta kama Danieli anamakosa yoyote. Walijaribu kumkosesha Danieli na Mfalme Dario. Wakuu wake walimchunguza Danieli kwa muda mrefu. Hawakumpata kwa makosa yoyote. Danieli alipenda na kumtumikia Mungu. Alikuwa mwaminifu. Hakuwa mfisadi wala mlegevu.

Danieli aliomba Mungu kila siku. Alipiga magoti kwa dirisha la nyumba yake na kuomba Mungu mara tatu kila siku. Wakuu wake hawakupata makosa yoyote kwa Danieli. Hawa wakuu wake wakafanya mpango muovu juu ya Danieli.

Wakuu wake walienda kwa Mfalme Dario. Walimwambia kwamba yeye Mfalme Dario ni mkuu sana. Walisema kwamba yeye ni kama mungu. Waliuliza mfalme Dario afanye sheria mpya. Wakuu wake walimuuliza Mfalme Dario afanye sheria ya kusema kwamba kwa siku 30, kila mtu lazima amwaabudu. Kwa siku 30 mtu yeyote asiabudu mungu mwingine. Lazima kila mtu aabudu Mfalme. Mtu yeyote atakayeabudu mungu mwingine atatupwa kwa tundu la simba.



Mfalme Dario hakujua kwamba huo mpango muovu ulikuwa juu ya Danieli. Aliona ilikuwa vizuri yeye kuwa kama mungu kwa siku 30. Mfalme Dario aliandika sheria mpya. Aliweka sahihi kwa hiyo sheria na akapiga muhuri. Sheria za Wamedi na Waajemi haingeweza kubadilishwa.

Danieli alisikia juu ya sheria mpya. Alijua adhabu kwa mtu atakayeomba Mungu. Danieli alipenda Mungu na alimwamini. Hakuacha kuomba Mungu. Danieli alienda kwa dirisha la nyumba yake. Alipiga magoti na kuomba Mungu. Danieli alikuwa jasiri sana. Aliamua kumtumikia Mungu. Danieli aliweka Mungu kwanza. Danieli alijua anaweza kufa lakini alikuwa mwaminifu kwa Mungu. Aliomba Mungu vile alikuwa akiomba kila siku. Aliuliza Mungu amsaidie.

Wakuu wale walienda kwa nyumba ya Danieli. Waliona Danieli akiomba Mungu. Wakuu wale walifurahi sana. Walienda kwa Mfalme Dario. Wakuu wake walimwambia Mfalme Dario, "Si ulifanya sheria kwamba mtu akiabudu mungu mwingine kando yako kwa siku 30, atatupwa ndani ya tundu la simba?" Mfalme alijibu, "Hiyo ndiyo sheria mpya. Kulingana na sheria za Wamedi na Waajemi, haiwezi kubadilishwa."

Halafu wakuu wale waliambia Mfalme, "Danieli hajaheshimu sheria. Anaomba Mungu wake mara tatu kwa siku." Mfalme Dario aliposikia hiyo, alifadhaika sana. Alifahamu kwamba huu ulikuwa mpango muovu uliopangiwa Danieli. Mfalme Dario alijua Danieli alikuwa mtu wa hekima na mzuri.

Alijaribu siku mzima kupata namna ya kumwokoa Danieli. Lakini sheria ya Wamedi na Waajemi haiwezi kubadilishwa. Ilipofika jioni wakuu wake walirudi kwa Mfalme Dario. Walimkumbusha Mfalme kwamba sheria haiwezi kubadilishwa. Mfalme alikasirika sana. Lakini hangeweza kubadilisha sheria. Mfalme Dario alituma wamuite Danieli. Danieli alikuwa mzee. Lakini alikuja kwa mfalme na ujasiri. Dario alijua Danieli alikuwa mwaminifu na ana ujasiri. Mfalme Dario aliambia Danieli, "Hebu Mungu, unayemtumikia akuokoe." Labda Mfalme Dario alikuwa amesikia vile Mungu aliokoa Shadraka, Meshaki na Abednego kutoka kwa moto. Alikuwa na tumaini kwamba Mungu ataokoa Danieli kutoka kwa simba.

Danieli alitupwa kwa tundu la simba. Jiwe lilifiringishwa na kufunika mdomo wa tundu. Mfalme na wakuu wake waliweka mihuri kwa jiwe na pete zao. Jiwe halingeweza kusongeshwa bila kuvunja mihuri.



Mfalme Dario alihangaika sana juu ya Danieli. Hakuweza kula. Hakuweza kulala. Usiku kucha alikuwa na wasi wasi juu ya Danieli.

Mapema kulipokuwa kumekucha, Mfalme Dario aliamka. Aliharakisha kwenda kwa tundu la simba. Jiwe lilikuwa bado na mihuri na kila kitu kilikuwa kimya. Mfalme aliita, "Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, Mungu wako ameweza kukuokoa kutoka kwa simba?"

Danieli alijibu, "Ee Mfalme, uishi milele! Mungu wangu alituma malaika. Malaika alishika midomo ya simba. Simba hawajanidhuru. Mungu alijua sikukuwa na makosa." Mfalme Dario alifurahi sana. Alituma watumishi wake kumtoa Danieli kutoka kwa tundu la simba. Danieli hakuumizwa hata, kwa sababu aliamini Mungu.

Mfalme Dario alikasikia wakuu wake waliofanya huu mpango muovu juu ya Danieli. Walitupwa wote katika tundu la simba.

Mfalme alifanya sheria mpya. Aliamrisha kwamba kila mtu aheshimu na kuogopa Mungu aliyeokoa Daniel kutoka kwa simba. Mfalme Dario alieneza hiyo amri mpya kwa Ufalme wake wote.